1 **UFAHAMU** (alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Siku hiyo Bi. Nyangweso aliwasili nyumbani muda mfupi kabla alama ya saa kugonga majira ya saa sita usiku kamili. Alitazama nyumba yake ilivyopangwa vizuri, kila kitu kimekaa mahali pake. Mandhari haya yaliufanya moyo wake kutua na tabasamu kubwa kumvaa. Mezani alitazama akaona vitabu vya mwanawe vimepangwa vizuri vikisubiri arauke na kuvitwaa kwenda shuleni. Aliridhika na kujihisi mwepesi mithili ya mtu aliyeutua mzigo mzito aliokuwa kabebeshwa masafa marefu.

Bi. Nyangweso alikuwa mteja maarufu wa mashirika mengi ya ndege yaliyompa huduma aliyohitaji. Alisafiri mara kwa mara ndani na nje ya nchi kwa ajili ya ajira yake iliyohitaji uwakilishi wake. Safari hizi zilimwezesha kukutana na marafiki wapya, hali kadhalika fursa mpya zilizompa changamoto na chagizo, si neno fursa zilikuja na mafungo gani. Aliona heri kuzikumbatia na kuzitumia vizuri walau apate kuuandalia vyema mustakabali wake na wa mwanawe.

Siku hiyo ya Bi. Nyangweso kurejea ilikuwa miezi miwili kamili tangu kuondoka kwake na kwenda ng'ambo kwa sababu ya mahitaji ya kikazi. Alikuwa **amekipeza** kitoto chake, na leo aliporudi tayari kilikuwa kimelala kitambo. Fikra zilimcheza shere na kumfanya kuduwaa. Upande mmoja ulimnasihi akiamshe huku mwingine ukimsimanga na kumsuta. Aliona heri akiamshe na wakati huo huo akaona atakidhulumu kwa, kukikatizia usingizi. Kwa kuwa siku iliyofuata ilikuwa siku ya kwenda skuli, aliona afadhali akiachie usingizi wacho na kurauka nacho kinapojiandaa kwenda skuli. Basi aliingia chumbani mwake akayakung'uta mablanketi yake kabla ya kukiachia kichwa chake kuudara mto.

Asubuhi ile alipoamka Bi. Nyangweso alikuta jua linakaribia kulingana. Mwanga wake ulikuwa umezagaa mwote chumbani kumfanya ashindwe kuona vizuri. Alishangaa jinsi usingizi ulivyomtwaa na kumfanya kupitiliwa kiasi kile. Hatimaye aliamka taratibu na kuelekea sebuleni ambapo alimkuta msichana wa kazi ametulia baada ya hekaheka za kupunguza kazi pale nyumbani. Mazungumzo yalipotamatisha kipindi cha salamu, Bi. Nyangweso alitaka kupata habari kuhusu mwanawe.

"Tuma, mwanangu vipi?'

"Hana neno ila siku moja alikuwa na joto jingi nikampeleka hospitali kupata dawa."

"Aah!" alimaka Bi. Nyangweso. "Iweje Tuma kwamba mwanangu, hili jicho moja, awe ameugua kiasi hicho wala usinidokezee katika mazungumzo yetu?"

www.kcse.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

"Si hivyo eti. Mimi niliona nitakuchanganya kukupa habari hizo. Mwenyewe umekuwa huko ughaibuni na shughuli zote hizo halafu nikuongeze na mengine? La hasha! Halikuwa kubwa la kukuhitaji wewe kuwepo wala kujua."

Bi. Nyangweso **aliyatia maneno yale katika mizani**. Aliyaona yenye ukweli mtupu. Alijua kuwa kazi zile alizopenda kujitolea kufanya zilikuwa taratibu zinamtenga na mwanawe. Japo alishukuru kuwa alikuwa na mtu mwema wa kumwangalia mwanawe, alimwonea wivu. Alianza kutambua kuwa Tuma alikuwa amechukua nafasi yake kama mzazi bila kumnyang'anya. Aliona kuwa mwanawe anakua bila yeye kuwa shahidi wa ukuaji wake. Mara ngapi amefanya kazi za shuleni na mwanawe kupitia *skype*? Mtandao uliwaunganisha vizuri wakazungumza karibu kila jioni kabla ya kuiaga siku, kwa hisani ya Tuma. Alikuwa akifurahi sana na kujihongera kwa mawasiliano na mwongozo wa kila siku kwa njia ya mtandao. Hata hivyo, sasa alianza kuona kuwa lilikuwepo pengo kubwa baina yake na mwanawe. Alijihisi mtupu moyoni. Alianza kuona mizani ya maisha ikielemea upande ambao hakuukusudia tangu hapo. Machozi yalimlengalenga naye akawa anafanya vita kuyazuia yasije yakamwagika mbele ya mwajiriwa wake.

(a) Eleza manufaa **matatu** ya safari kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(b) "Tuma amewajibika." Thibitisha kwa hoja **tano**. (alama 5)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(c) Fafanua changamoto **tano** zinazoweza kuzikumba familia zenye wazazi wanaofanya kazi ya ajira kwa mujibu wa kifungu. (alama 5)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

(d) Eleza maana za maneno haya kwa mujibu wa kifungu. (alama 2)

(i) **amekipeza** ..........................................................................................................

(ii) **aliyatia maneno yale katika mizani**

..........................................................................................................

1

2 **UFUPISHO** (alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tabasamu ni miongoni mwa vitu ambavyo tunavishiriki siku baada ya siku lakini ambavyo hatuvitambui sana. Ni muhali siku kupita bila mtu kutabasamu. Hili ni jambo ambalo aghalabu hutokea pasi na kupangwa. Tabasamu hujialika na kujivisha kwenye midomo ya watu hasa wanapofurahi. Mtu anapotabasamu inabashirika kuwa analipokea jambo au mtu kwa uzuri. Utafiti wa kisayansi umebaini kuwa tabasamu zina faida kubwa kwa mwanadamu.

Je, wajua kwamba tabasamu humfanya mtu kupendeza na hivyo kuwavutia wengine? Kuna tofauti kubwa kati ya mtu mwenye desturi ya kutabasamu na yule ambaye uso wake ni mkavu kama jabali. Utaona kuwa ni rahisi kumchangamkia mtu ajinabi kwa sababu ya kutabasamu na kumwambaa ndugu ambaye ni bahili wa tabasamu. Upo mvuto wa nje unaoshawishi fikra zetu kuhusu watu wenye kutabasamu na vilevile sura ya nje inayotufanya kujibari na watu wasioachia tabasamu. Ishara za mwili kama vile kukunyaa huwafanya watu kumkwepa aliyenazo. Dawa nzuri isiyo na gharama ya kuwafanya watu kukuchangamkia ni kupitia kwa tabasamu zetu.

Katika ulimwengu wenye hekaheka na shauku nyingi, watu hujikuta katika tatizo la msongo wa mawazo. Nyuso zetu zinaweza kusaliti hali zetu na kuzidhihirisha. Hivyo basi tabasamu hutusaidia kwa kutukinga dhidi ya kuonekana wachovu, kulemewa au kuzidiwa. Zaidi ya hayo, tabasamu hutuwezesha kupunguza msongo wa mawazo hata pale tunapotabasamu bila kutaka au kwa kutabasamu bila kufahamu. Unapokuwa na msongo wa mawazo, jaribu kutabasamu. Tabasamu yako itakufaidi wewe na wale ulionao. Tabasamu hukujaza nguvu hata pale unapokuwa ukikabiliwa na hali tata. Hata tabasamu inapokuwa imelazimishwa huwa bado inatuma ujumbe wa kuushawishi ubongo na sehemu nyingine za mwili kuwa maisha yanapendeza.

Mtu anapokuwa amezidiwa na huzuni, anaweza kurudi katika hali ya uchangamfu kwa kutabasamu. Kuna uwezekano mkubwa wa hali hiyo ya huzuni kumtoka na kujawa na uchangamfu. Tabasamu huhadaa mwili na kumsaidia mtu kuchangamka kwa sababu tendo la kutabasamu huziamsha neva za ubongo zinazohusika na habari katika ubongo.

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

Tabasamu inaweza kufananishwa na moto katika kichaka kikavu ambao husambaa na kuathiri vyote vilivyo karibu nao. Nguvu za tabasamu ni kubwa. Mtu anapowapa wengine tabasamu, huwafanya kuchangamka na kufanya hali kupendeza zaidi. Mazingira yoyote ambapo watu wana mazoea ya kutabasamu hupendeza na huacha athari ya kudumu kwa watu. Nayo mazingira yasiyo na tabasamu, hata kama hayana ubaya wowote, huweza kuhisika kuwa magumu, masumbufu na yenye kuchosha. Hapana shaka basi kuwa, tabasamu ina athari kubwa kwa anayeitoa na anayeipokea.

Wataalamu wamebaini kuwa tabasamu ni jambo muhimu katika afya ya mtu. Tabasamu huweza kuimarisha afya kwa jumla. Mfumo wa kupambana na magonjwa katika mwili wa mwanadamu huwezeshwa kufanya kazi vyema zaidi. Inachukuliwa kuwa, kwa kutabasamu mfumo wa kupambana na magonjwa katika mwili wa binadamu huimarika kwa sababu mtu huwa yumo katika hali ya utulivu zaidi. Mbali na kuchukua tahadhari dhidi ya homa kwa kunawa mikono, unaweza pia kutahadhari kwa kutabasamu.` Kuhusu suala hili la afya, imebainika kuwa tatizo la shinikizo la damu linaweza kukabiliwa kwa kutabasamu. Shinikizo la damu linapokuwa juu, tabasamu ina uwezo wa kulirudisha chini.

Una habari kuwa tabasamu humfanya mtu kuhisi vizuri? Tabasamu huchochea mwili kutoa kemikali ambazo huleta uchangamfu. Aidha, kemikali hizo hufanya mwili kulainika na kupunguza maumivu. Kwa kufanya hivi, tabasamu huwa ni dawa asili ya mwili. Vivyo hivyo tabasamu humfanya mtu kupendeza na kumpa sura ya ujana. Mishipa inayotumika kutoa tabasamu pia huimarisha uso na kumfanya mtu kuonekana kijana zaidi. Hivyo, hata wale ambao hawatumii vipodozi kuutengeneza uso wanaweza kujaribu kutabasamu kiasi kikubwa cha siku. Hili litawafanya waonekane kuwa kijana zaidi na kujisikia vyema zaidi.

Manufaa ya tabasamu ni mengi. Mathalani utafiti umeonyesha kuwa watu wanaotabasamu mara kwa mara huonekana kuwa wakakamavu. Watu hao wana nafasi nzuri ya kupanda ngazi kazini na ni rahisi kwa watu wengine kuwaendea au kutangamana nao. Inafaa kujaribu kutabasamu katika vikao na mikutano ya kibiashara. Ukifanya hivyo unaweza kuona watu wanavyokupokea kwa namna tofauti.

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

(a) Fupisha aya tano za mwanzo kwa maneno 120. (alama 9)

**Matayarisho**

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

**Nakala Safi**

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

(b) Eleza masuala ambayo mwandishi ameibua katika aya **tatu** za mwisho kwa maneno 70. (alama 6 )

**Matayarisho**

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

**Nakala Safi**

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

**3 MATUMIZI YA LUGHA** (alama 40)

(a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (alama 2)

(i) konsonanti konsonanti irabu + konsonanti irabu

..............................................................................................................................

(ii) irabu + konsonanti irabu + irabu

..............................................................................................................................

(b) Bainisha silabi katika neno: changamka (alama 1)

..............................................................................................................................

(c) Eleza majukumu ya viambishi katika neno:

wanaojenga (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(d) Eleza aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi:

Yule **mwingine** **ataweza** kujiunga **nao** **mwakani.** (alama 2

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(e) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya umoja. (alama 2

Wanagenzi hao walinadhifisha maabara na karakana vyuoni.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(f) Akifisha sentensi ifuatayo:

Mwalimu wetu bw Ndala ni mtaalamu wa tamthilia mchezo wa kuigiza (alama 2

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

3(9)



(g) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo. (alama 3)

(i) Sika humwogopa mbwa wa jirani.

(Anza kwa: Mbwa ...)

..............................................................................................................................................

(ii) Viongozi **wakiwajibika**, uchumi wa taifa utaimarika.

(Badilisha kitenzi kilichopigiwa mstari kuwa nomino.)

..............................................................................................................................................

(iii) Baraka anafanya biashara ya kuuza mboga na matunda.
Baraka amefuga ng'ombe wengi wa gredi.

(Unganisha kuwa sentensi moja bila kutumia kiunganishi.)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

h) Tunga sentensi **tatu** kuonyesha matumizi **matatu** ya kiambishi **-ki-** (alama 3)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

(i) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 2)

Ngoma mpya ilipochezwa, mji wote ulichangamka.

..............................................................................................................................................

(j) Geuza sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya kuendelea. (alama 2)

Barabara nyingi ziliteleza mvua ilipoanza kunyesha.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

(k) Ainisha sentensi zifuatazo ukizingatia uamilifu wake.

(i) Kaleteni vyombo vyote vya muziki. (alama 1)

.................................................................................................................................

(ii) Tafadhali mletee mgonjwa dawa. (alama 1)

.................................................................................................................................

(l) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kukanusha.

Mkulima huamka alfajiri na kuandaa kiamsha kinywa. (alama 2)

.................................................................................................................................

(m) Bainisha matumizi ya 'ndi' katika sentensi:

Jamala ndiye aliyetupigia chapa makala hayo. (alama 1)

.................................................................................................................................

(n) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo:

Kampuni hii inatarajia faida kubwa mwakani. (alama 2)

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

(o) Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo:

(i) $S_1 \rightarrow KN(N) + KT(T) + U + S_2 \rightarrow KN(N) + KT(T+E)$ (alama 2)

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

(ii) $S \rightarrow KN(Ø) + KT(T + N)$ (alama 1)

.................................................................................................................................

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

(p) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **suka** na **zuka.** (alama 2)

..............................................................................................................................

(q) Kubali ni kwa kataa ilhali zama ni kwa ______________. (alama 1)

(r) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari.

Kijana **mvumilivu** **amepewa** zawadi nzuri. (alama 2)

..............................................................................................................................

(s) Robota ni fungu la nguo ilhali __________________ ni kundi la vifaranga. (alama 1)

..............................................................................................................................

(t) Kaza roho ni kwa kujitahidi kufanya jambo na ______________________________ ni kwa kukosa kupata ulichodhamiria. (alama 1)

(u) Dinda alibandika chungu cha mboga akaenda kucheza na wenzake. Aliporudi alipata mboga zimeungua na kugeuka makaa. Andika methali inayoweza kutumiwa kuelezea hali hii.

(alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner

## 4 ISIMUJAMII (alama 10)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

**Mwenyekiti:** Karibu Bwana Mwamba. Keti.
Naomba ulipitishie jopo hili stakabadhi zako ...
Naam Bwana Mwamba jitambulishe kwa jopo hili.

**Mwamba:** Mimi ninaitwa Maarifa Mwamba. Nimehitimu shahada ya uzamifu katika usimamizi wa fedha kutoka Chuo Kikuu cha Tegemeo.
Nimefanya kazi kama Mkurugenzi wa masuala ya usimamizi wa fedha katika Shirika la Teknolojia ya Mawasiliano la Mbalamwezi. Nina tajriba ya miaka kumi katika usimamizi wa fedha. Nina uwezo wa kutekeleza majukumu yangu bila kusimamiwa.

**Mwenyekiti:** Shukran Dkt. Mwamba. Je, unatarajia kutoa mchango upi kuimarisha utendakazi katika shirika hili iwapo utapata nafasi ya kazi uliyoiomba?

(a) Bainisha sajili ya makala haya. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(b) Eleza sifa **nane** za sajili hii kwa kurejelea makala haya. (alama 8)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

www.kala.co.ke

Scanned with OKEN Scanner